

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA GHARAMA ZA UJENZI WA BOMBA LA GESI NA MITAMBO YA KUCHAKATA GESI - MADIMBA (MTWARA) NA SONGO SONGO (LINDI)

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linapenda kutoa taarifa ya gharama halisi za mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) hadi Dar es Salaam.

Taarifa hii inalenga kufafanua gharama halisi za mradi tangu kuanza kwake mwaka 2013 hadi kukamilika mwaka 2015.

Mradi huu umetekelezwa kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya watu wa China. Jumla ya gharama za ujenzi wa mradi kwa fedha za kigeni ni Dola za Marekani zipatazo bilioni 1.225, ambapo asilimia 95 ni mkopo na asilimia 5 ni mchango wa Serikali ya Tanzania.

Gharama hizi kwa fedha za kigeni zimegawanyika kama ifuatavyo:

- a) Mtambo wa kuchakata gesi asilia wa Songo Songo Dola za Marekani **151,735,000;**
- b) Mtambo wa kuchakata gesi asilia wa Mnazi Bay Dola za Marekani **197,877,000;**
- c) Bomba la kusafirisha gesi asilia Dola za Marekani **875,715,000.**

Hata hivyo, zipo gharama nyingine ambazo Serikali imeendelea kuzibeba nje ya asilimia 5 zinazotajwa hapo juu. Gharama hizi ni pamoja na zile za upatikanaji wa Mkuza wa Bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu, usimamizi wa mradi, gharama za kuagiza mitambo ya "compressors" kwa ajili ya Songo Songo; Kazi za ziada za Mkandarasi; gharama za kuongeza upana wa Mkuza kutoka Somanga Fungu hadi Tegeta; gharama za kununua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia pamoja na maeneo ya ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi na hivyo kufanya gharama zote za mradi kufikia Dola za Marekani **bilioni 1.3.**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linapenda kuchukua fursa hii kusisitiza kuwa gharama zilizooneshwa hapo juu ndio gharama halisi za mradi na si vinginevyo. TPDC ipo tayari wakati wowote kutoa ufafanuzi utakaohitajika kutokana na taarifa iliyoelezwa hapo juu.

**IMETOLEWA NA:
OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA**